

## Maswali

1. Mbona Mungu alikasirikia Mfalme Ahabu?
2. Mungu alimtuma nani kwa Mfalme Ahabu?
3. Eliya aliambia Mfalme Ahabu nini?
4. Nani alimlinda Eliya?
5. Mungu alimtuma Eliya wapi?
6. Eliya alipata chakula namna gani kila siku?
7. Mungu alimtuma Eliya wapi kijito kilipokauka?
8. Mwanamke mjane alikuwa amebaki na chakula kiasi gani?
9. Eliya, mwanamke mjane na mwanawe walipata chakula namna gani kila siku?
10. Eliya alifanya nini mwana wa mwanamke mjane alipokufa? Nini ilifanyika?

## Majibu

1. Ahabu na watu wote waliabudu Baali.
2. Mungu amlituma Eliya kwa Ahabu.
3. Hakutakuwa na mvua. Hakuna chakula kitakua. Kutakuwa na njaa.
4. Mungu alimlinda Eliya.
5. Mungu alimtuma Eliya kuishi karibu na Kijito cha Kerithi.
6. Kunguru walimletea mkate na nyama kila asubuhi na jioni.
7. Mungu alituma Eliya Sarepta.
8. Alikuwa na konzi la unga na mafuta kidogo kwa chupa.
9. Unga na mafuta havikuisha. Mungu aliwalinda kwa hivyo ali-waletea.
10. Eliya aliomba Mungu. Mungu alisikia maombi ya Eliya na akamrudishia yule mtoto uhai.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1   Mwaka wa 3**



## 30 Mungu analisha Eliya

### Marejeo

1 Wafalme mlango wa 17

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anapeana wale wanaompenda, wanaomwamini na wanaomtii.

### Maneno maalum

- 30.1 Eliya + nabii + Mfalme Ahabu + muovu + abudu Baali + Mungu anakasirika
- 30.2 Mungu + Eliya + Mfalme Ahabu + hakuna mvua + mito zikakauka + hakuna chakula + Mungu anajali + Eliya + kijito cha Kerithi + kunguru + mkate na nyama
- 30.3 Kijito kilikauka + Mungu hujali + Sarepta + mwanamke mjane + konzi la unga + mafuta kidogo + mzuri + tengeneza mkate + kila siku unga na mafuta
30. 4 Mwana mgonjwa + Eliya aliomba + Mungu alisikia + mtoto hai + shukuru Mungu

**30.1** Eliya alikuwa nabii. Alifundisha watu maneno ya Mungu na kuwaambia yote yatakayokuweko siku za baadaye.

Mfalme Ahabu alikuwa mwovu sana. Aliabudu Baali, mungu wa uongo. Alifundisha watu kuabudu Baali. Mungu alikasirika kwa sababu Ahabu na watu wake waliabudu Baali.

**30.2** Mungu alituma Eliya kuambia Mfalme Ahabu kwamba atamwadhibu yeye Ahabu na Waisraeli wote. Eliya aliambia Mfalme Ahabu kwamba Mungu hatatuma mvua kabisa mpaka yeye Eliya aseme kwamba inyeshe. Mito yote itakauka na hakutakuwa na mimea ya kukua. Hakuna mtu atakuwa na chakula cha kutosha.

Kwa hivyo hakukuwa na mvua na kila mtu alikuwa na kiu na njaa. Lakini Mungu alikuwa akilinda Eliya. Mungu alimwambia aende kwa Kijito cha Kerithi. Atapata maji ya kunywa kule. Mungu alituma ndege wakubwa weusi waitwao kunguru, waletee Eliya chakula. Kwa hivyo Eliya aliishi kwa Kijito cha Kerithi kwa miezi gadhaa. Alikunywa maji kutoka kwa Kijito. Kila asubuhi na jioni, kunguru walimletea mkate na nyama kwa midomo yao.



**30.3** Baada ya muda mrefu maji ya kijito ilianza kukauka. Siku moja kukawa hakuna maji kabisa. Eliya hakuogopa kwa sababu alijua Mungu atamlinda. Mungu alizungumza na Eliya na kumwambia aende kwa mji uitwao Sarepta. Kule atapata mwanamke mjane, yeye ndiye atampa chakula cha kukula.

Eliya alipofika Sarepta alimwona yule mwanamke mjane. Eliya alikuwa na njaa na kiu sana baada ya safari yake ndefu kwa hivyo aliuliza yule mwanamke mjane ampe chakula na kinywaji.



Lakini mwanamke mjane alitigiza kichwa na kusema, "Nina konzi la unga na mafuta kidogo kwa chupa. Ninaokota kuni niende niwashe moto ili nitengeneze mkate kidogo tule mimi na mwanangu halafu tufe."

Eliya aliambia mwanamke mjane kwamba asiogope lakini kwanza amtengenezee yeye mkate kidogo. Mungu atamlinda yeye na mwanawе akifanya hivyo. Mwanamke mjane alikuwa mzuri na aliamini neno la Mungu. Alitumia unga na mafuta yake kutengenezea Eliya mkate kwanza. Baadaye, bado kulikuwa na unga na mafuta ya kutosha kutengenezea yeye na mwanawе.

Eliya alikaa na mwanamke mjane kwa muda mrefu. Kila siku mwanamke mjane alitengeneza mkate kidogo yake, mwanawе na Eliya kutoka kwa hiyo konzi la unga na chupa ya mafuta. Unga na mafuta hazikuisha. Wakati wote baada ya kupika bado kulikuwa na kiasi cha kutosha. Mungu alilinda Eliya, na mwanamke mjane na mwanawе kwa muda mrefu.

**30.4** Halafu, siku moja, mwana wa mwanamke mjane alikuwa mgonjwa sana. Aliendelea kuwa mgonjwa na kuwa vibaya na baadaye akafa. Mwanamke mjane alihuzunika sana. Eliya alimpeleka kwa orofa na kumlaza kwa kitanda chake.

Eliya aliomba Mungu na kumuuliza amponye na amrudishie uhai. Eliya alilala juu ya kijana na kumpulizia hewa kwa mdomo wake. Alirudia hivyo mara tatu na akaomba Mungu tena.

Mungu alisikia maombi ya Eliya na kijana alifungua macho na kuamka pole pole. Eliya aliteremsha kijani chini kwa mama yake akiwa mzima na mama alifurahi sana alipoona mtoto wake hai tena. Alishukuru Mungu na Eliya sana. Alisema, "Sasa najua kweli wewe ni nabii wa Mungu. Ninajua maneno yako kutoka kwa Mungu ni kweli."